Jedwali la 6: Muundo wa Madaraja kwa Kutumia Pointi (CSEE)

DARAJA	POINTI/VIGEZO CSEE	POINTI/VIGEZO ACSEE
I	7 – 17	3 – 7
II	18 – 24	8 – 9
III	25 – 31	10- 13
IV	Awe na **angalau D** mbili au *Credit Pass* moja isiyopungua **C**.	Awe na **angalau D** mbili au *Principal Pass* moja isiyopungua **C**.
O	Aliyepata ufaulu chini ya **D** mbili	Aliyepata ufaulu chini ya **D** mbili

Ambapo pointi kwa kila gredi ni kama ifuatavyo:
A = 1, B+ = 2, B = 3, C= 4, D = 5, E = 6 na F = 7

Mfano:

a) Kwa mtahiniwa wa CSEE aliyepata matokeo yaliyoainishwa hapa chini atakuwa na idadi ya pointi katika masomo saba aliyofaulu vizuri zaidi kama ilivyooneshwa katika Jedwali lifuatalo:

SOMO	Civ.	Hist.	Geog.	Kisw.	English	Phy.	Chem.	Biol.	Maths	Pointi
GRADE	A	B+	B+	B	C	C	C	C	E	
UZITO WA GREDI	1	2	2	3	4	4	4	4	6	**20**

Idadi ya Pointi alizopata katika masomo Saba aliyofanya vizuri zaidi ni **1 + 2+ 2 + 3 + 4+ 4 + 4 = = 20**

Hivyo, kwa Pointi **20**, mtahiniwa anatunukiwa matokeo yenye **Division Two.**

b) Kwa mtahiniwa wa ACSEE aliyepata matokeo yaliyoainishwa hapa chini atakuwa na idadi ya pointi katika masomo ya tahasusi kama ilivyooneshwa katika Jedwali lifuatalo:

MASOMO	Tahasusi (combination)			Ziada		Pointi
	Phy.	Chem.	Biol.	BAM	GS	
GRADE	E	B+	A	D	A	
UZITO WA GREDI	6	2	1	5	1	**9**

Idadi ya Pointi alizopata katika masomo ya tahasusi (combination subjects) ni **6 + 2+ 1 = 9.**

Hivyo, kwa Pointi **9**, mtahiniwa huyu hutunukiwa matokeo yenye **Division Two.**

3.4.2 Madaraja katika Mfumo wa GPA

'*Grade Point Average*' (GPA) ni Mfumo wa Kutunuku ambao huonesha wastani wa pointi alizopata mtahiniwa katika masomo aliyofaulu katika mtihani wake. Madaraja katika mfumo wa GPA hupangwa katika utaratibu wa *Distinction, Merit, Credit* na *Pass* ambapo daraja la *Distinction* ni la ufaulu wa juu zaidi na daraja la *Pass* ni la ufaulu wa chini. Mtahiniwa hutunukiwa Gredi A, B$^+$, B, C, D, E au F kutegemeana na ufaulu wake katika somo ambapo uzito wa alama katika gredi **A = 5, B$^+$ = 4, B = 3, C=2, D = 1, E = 0.5** na **F = 0**. Mtahiniwa atahesabiwa kuwa amefaulu somo endapo atapata Gredi **D** ambayo ni sawa na uzito wa **Pointi 1**.

Ukokotoaji wa jumla ya GPA ya mtahiniwa hufanyika kwa kuzingatia masomo ambayo mtahiniwa amefaulu angalau kwa Gredi D na kuendelea (D, C, B, B+ na A). GPA anayopata mtahiniwa hutokana na wastani wa pointi alizopata katika masomo saba aliyofanya vizuri zaidi kwa Mtihani wa Kidato cha Nne au masomo matatu ya tahasusi kwa Mtihani wa Kidato cha Sita. Aidha, GPA ya mtahiniwa huandikwa katika nafasi moja ya Desimali ambapo nafasi ya pili ya desimali hukadiriwa katika makumi yaliyokaribu. Mfano, mtahiniwa mwenye GPA ya 3.15 itakuwa sawa na 3.2 na mtahiniwa mwenye GPA ya 3.14 itakuwa sawa na 3.1.

Muundo wa madaraja kwa kutumia GPA katika Mitihani ya Kidato cha Nne na cha Sita ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali la 7.

Jedwali la 7: Muundo wa Madaraja kwa Kutumia GPA

DARAJA	CSEE	ACSEE
Distinction	3.6-5.0	3.7-5.0
Merit	2.6-3.5	3.0-3.6
Credit	1.6-2.5	1.7-2.9
Pass	0.3-1.5	0.7-1.6
Fail	0.0-0.2	0.0-0.6